

IMANI YA MARIAMU



U hali gani, Ndugu Moore? Asante, Ndugu.

² Hakika ilikuwa, sina budi kusema, “Amina,” kwa hilo, Bwana alitubariki asubuhi ya leo kwa njia isiyo ya kawaida kabisa. Nilikuwa na jambo fulani niani mwangu nililotaka kuzungumzia, kisha nikalibadilisha tu mara moja, na hiyo ndiyo aina ya mikutano ninayopenda, huo utamu wa Roho Mtakatifu ukiingia tu, ukitiririka kote jengoni.

³ Halafu basi, Roho Mtakatifu, jana usiku, nadhani hapana shaka ilikuwa ni unabii, nilisema wahudumu nyuma yangu, ya kwamba wakati wao ungekuja, walikuwa wakijitolea, na asubuhi ya leo, mbona, kabla hata sijaanza, angalau, wema wa Roho Mtakatifu ukaenda moja kwa moja miongoni mwa wahudumu hao, ukawatangaza wameponywa, moja kwa moja kote kupitia pale, kuwaambia hali zao, na magonjwa, na kadhalika. Loo, Yeye ni mwema, sivyo? Yeye hakika, Yeye ni Baba wa ajabu, tunashukuru sana kwa ajili Yake.

⁴ Na sasa, kesho alasiri, Bwana akipenda, tutabadilisha ibada kutoka kesho usiku, mpaka kesho alasiri. Nami nafikiri hilo ni zuri, linampa kila mtu nafasi ya kuendeleza makanisa yao. Daima nafikiri ni wajibu wa Mkristo kusimama kwenye wajibu wake. Na kwa njia hiyo, wakati tunapokuwa na m—mkutano kama huu, mbona, na ndugu ambao wako tayari kufunga makanisa yao na kuwatuma watu wao huku, ninawaambia ninyi wageni wote hapa sasa, mlio hapa nje ya mji na mbali na makanisa haya, nendeni kanisani kesho, jichagulie tu.

⁵ Kuna kundi zuri la ndugu hapa, na makanisa mazuri yanayoamini Injili ii hii tunayohubiri. Wamesimama hapa, nao ni, watafurahi kuwa pamoja nanyi kwenye shule zao za Jumapili kesho asubuhi, na makanisa yao kesho usiku. Na sasa, hakikisheni mnahudhuria kanisa fulani, kanisa mnalojichagulia.

⁶ Nadhani ndugu wamewaambia ambapo walifanya maandalizi ya namna fulani, kusema mahali walipo na yote juu yake; kwa kawaida wao hufanya hivyo. Nanyi mmealikwa kwa yote hayo. Na kwa hiyo sasa kanisa, popote utakapoenda kanisani, lile unalowakilisha, chochote unachotaka kufanya, vema hilo—hilo litakuwa sawa tu.

⁷ Sasa, ninawaona wakiingia kwenye sinema, ama kitu fulani. Kwa hiyo, kuna Roho mkuu miongoni mwa watu, uamsho mkuu unaonekana unaelekea huku. Ninatumaini kamwe hautampoteza Roho huyo mzuri aliyekuwa mkutanoni asubuhi ya leo. Hilo—hilo kweli ni jambo fulani unapoona wema

wa Mungu na rehema Zake zikija na kutubariki, na kufanya mambo aliyofanya asubuhi ya leo.

⁸ Sasa, Bwana akipenda, kesho alasiri ninataka kuufanya ninii, kama mkutano m—mzuri wa Kikristo, na kuacha tu kila mtu atoke. Tutahubiri tu mahubiri ya kiinjalisti kesho alasiri, Bwana akipenda. Naye Ndugu Leo, mtu wetu wa vitabu, alisema, “Ndugu Branham, unapaswa kuhubiri wakati mmoja hapa chini kwa watu hawa kama yale mahubiri ya mtindo wa kale.”

⁹ Bwana kwa kuwa ni mwema kwetu, tunawatakeni mfungue Biblia zenu mkitaka, ama mwandike tu hili somo, nina kifungu kimoja tu cha kusoma, katika Luka, mlango wa kwanza, kifungu cha 37:

Kwa maana hakuna neno lisilowezezana kwa Mungu.

Mariamumu akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema. Kisha malaika akaondoka akaenda zake.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

¹⁰ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja katika Jina la Bwana Yesu kuomba rehema na msamaha kwa mapungufu yetu. Tungeomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba ungeendelea kututembelea katika kujiliwa huku kukuu kwa Roho Wako Mtakatifu, upate kujionyesha Mwenyewe hai mpaka utakapoonekana tena katika umbo la kimwili katika kule Kuja mara ya Pili.

¹¹ Tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba kama kungekuwako na yeyote miongoni mwetu ambaye hajawahi kukukubali Wewe kama Mwokozi wao mpendwa, mwenye upendo kwamba usiku wa leo utakuwa ndio wakati ule ambapo watafanya ule utoshelezao kwa yote, “Naam, Bwana, ninaamini.” Wale ambao wameanza hivyo na bado hawajaufikia ubatizo wa Roho, tunaomba ya kwamba wao, pia, watajalisalimisha, usiku wa leo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

¹² Jana jioni tulifurahi sana, Bwana, kukuona ukitoka kwenda miongoni mwa watu, wale walioinua mikono yao kwamba hawakuwa na kadi za maombi, tukamwona Roho Wako Mtakatifu mkuu akitokea na kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka, na kuwaita, akifanya kama tu ulivyofanya wakati alipoishi katika Mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo, ikionyesha ya kwamba Wewe ungali Kanisani Mwako, watu wakisimama kutoka kwenye machela na kwenda zao, na wale waliokuwa wakifa, kwenye tumaini la mwisho, waliiona Nuru ya Mungu na kuikubali, wakaondoka wameponywa. Ule mkutano mkuu asubuhi ya leo katika ushirika pamoja na Roho Mtakatifu, tunapoketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, Ee Mungu, jinsi tunavyopenda hilo!

¹³ Nasi tunaomba ya kwamba utatupa baraka Zako za Kimbinguni usiku wa leo. Usiangalie kutostahili kwetu, Bwana,

kwa sababu hatustahili, wala hakuna kitu ambacho tungeweza kufanya kustahili chochote. Kwa hiyo tunakiri kwa unyenyekevu kwamba sisi—sisi tu wakosaji, nasi ni waovu, na Wewe pekee ndiwe mwenye haki, nasi tunakuja katika Jina la Bwana Yesu, kama Yeye alivyotuagiza kuja, akiahidi ya kwamba tungepata kile tunachoomba.

¹⁴ Mungu, nitakuomba jambo kuu, nami ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atachunguza kila moyo hapa usiku wa leo, kama wanahitaji uponyaji, waponye, Bwana, chochote wanachohitaji, wajalie, Bwana, wala usinisahau hapa nyuma, usisahau kundi hili zuri la wahudumu, Bwana.

¹⁵ Yabariki makanisa yao kesho, jalia kuweko, yajae tu kabisa, huku Roho wa Mungu akitenda kazi kupitia kwao. Jalia utokee uamsho wa mtindo wa kale katika nchi hii hapa, na kuenea tu kote katika taifa. Wabariki watu wote kila mahali, Baba. Sasa, nilivyosoma maneno haya machache, ninaomba ya kwamba utayabariki mioyoni mwetu. Tunaomba, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

¹⁶ Jua la asubuhi lilikuwa tu likichomoza juu ya kilima alipokuwa akitembea kwenye barabara ndogo, inayojulikana, akishuka kilima alikoishi. Naye alipokuwa akitembea na mtungi wa maji chini ya mkono wake, labda alikuwa akiwazia, akitafakari, kama wasichana kwa kawaida, yapata umri huo, wanavyoweza kutembea wakitafakari, naye alikuwa akienda zake kwenye kisima cha mjini kupata ugavi wa kila siku wa maji. Tunaambiwa ya kwamba mama yake alikuwa amekufa, kwa hiyo kwa namna fulani aliitunza nyumba pale peke yake na baba yake mzee. Naye alikuwa akiwazia juu ya siku iliyotangulia.

¹⁷ Hapana shaka ilikuwa katika siku ya kwanza ya juma, baada ya kufanya ibada ya Sabato, nalo jua likichomoza vizuri sana na kupanda kwenye zile anga za bluu za Palestina. Na uzuri wa maua wakati jua linapochomoza, mazingira hayo, harufu hiyo nzuri ya maua na maua-asali, wakati joto likiyanyausha, saa chache tu kabla halijayakausha kabisa tena, ninapenda wakati huo wa asubuhi, nafikiri ni mpya. Ninapenda kutoka nje bustanini.

¹⁸ Nafikiri mhudumu anapaswa kuja jukwaani, si huku amelemewa na mizigo mingi, bali kutoka kwenye upya wa Uwepo wa Bwana. Aondoke asubuhi na mapema pepo wote wakisha kwenda kulala, na makelele ya usiku karibu yamekwisha, ndipo kunatulua na kuwa kimya, na kunusa harufu hiyo nzuri, huo utamu. Nami naamini kama mhudumu angekaa tu mbele za Mungu mpaka aingie mimbarani, angekuja kama harufu nzuri, ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu kuuleta ujumbe wa Mungu kwa watu wenye mioyo yenye njaa wanaongojea.

¹⁹ Alipokuwa akishuka njiani, naamini, ama, huenda nikasema hili kama mchezo mdogo wa kuigiza, kwamba alikuwa akitafakari juu ya kile kilichotukia siku iliyotangulia. Wakiisha kutoka kanisani, mbona, ilikuwa ni desturi kwamba mumewe aliyemposa, Yusufu, alikuwa aje nyumbani pamoja naye siku hiyo kwa chakula cha kutwa. Na chakula cha kutwa kilipoandaliwa, mbona, walikuwa wamekula chakula chao cha kutwa, na kama kawaida, wakaketi barazani, wakiangalia ng'ambo ya maskini lile bonde upande wa pili wa kilima.

²⁰ Yusufu alikuwa seremala, na akijua ya kwamba alikuwa akijiandaa kumwoa msichana huyu mrembo Myahudi, akiwa seremala, alikuwa akijenga makazi yao ya baadaye kwenye kilima hicho kingine. Kwa hiyo ninii, mwajua, ningewazia ilibidi ipate mguso huo mdogo maalum kwake, kwa sababu alikuwa anataka kumleta bibi-arusi wake mdogo mrembo, katika nyumba hii, nayo milango ilipaswa kutoshea vizuri kabisa.

²¹ Na—naye alikuwa akichukua wakati wake kufanya hivyo, kwa sababu hakutaka kazi ya haraka kwa hili. Hana budi kuwa... Madirisha hayana budi kutoshea vizuri kabisa, na milango iwe sawa kabisa. Ningewazia wakati alipoingia langoni, huenda lilikuwa la umbo kubwa la moyo, ili kwamba wakati alipoingia, atengeneze hilo lango katika umbo la moyo, na maua ya waridi kote kuizunguka nyumba. Nao walikuwa wamepanga jambo hili kwa muda, tangu uchumba wao.

²² Nao wangetoka waende kule, tuseme, Jumapili alasiri, na kuketi chini barazani, na kuangalia ng'ambo ya pili ambapo makazi yao ya baadaye yangukuwa, na kama desturi wangenena habari za Bwana, kwa sababu wote wawili walikuwa waaminio hodari wa Mungu.

²³ Basi Jumapili hii ilikuwa ni ya kipekee. Huku wakiharakisha chakula cha kutwa, na kuosha vyombo, naye Yusufu alikuwa tayari ameketi barazani wakati Mariamu alipowasili, na—na hapana shaka yalikuwa ni maongezi ya kitu kama hiki, kwa kuwa kwa kawaida walizungumza juu ya jinsi nyumba ilivyokuwa imejengwa, na jinsi tu ingeonekana, nao marabi wangukuja pamoja nao nyumbani kwa chakula cha kutwa, lakini badala yake, wakaangukia somo la ujumbe wa asubuhi hiyo ambao walikuwa wamesikia kutoka kwa rabi, yule mtu mashuhuri, msheshimiwa.

Na labda Mariamu ndiye aliyesema, “Yusufu, huo si ulikuwa ujumbe wa kuvutia sana asubuhi ya leo ambao rabi aliuhubiri, mchungaji wetu mpendwa?”

²⁴ “Loo,” hapana shaka Yusufu alisema, “huo ulikuwa ni ujumbe mzuri sana! Niliupenda sana aliponena juu ya Yehova yule Mungu mkuu, aliyewaongoza watu wetu kutoka Misri. Hivi haikukuchangamsha sana aliposoma yale Magombo ya Kutoka

wakati walipotolewa, na jinsi ambavyo Yehova aliwaongoza kwa Nguzo ya Moto? Nao hawakuwa na dira ya kwenda, bali walifuata uongozi wa Roho. Loo, Mariamu, si ingekuwa ni ajabu kama tungeweza kuishi maisha yetu yote tukiiangalia hiyo Nguzo ya Moto na kuongozwa jinsi walivyoongozwa?

²⁵ “Na jinsi ambavyo walipohitaji chakula, Yeye alinyesha mana kutoka Mbinguni, wakawa na mkate; kisha walipohitaji nyama, Yeye aliwanyeshea kware kutoka pwani, wakaijaza nchi, na walipohitaji maji, Yeye alikuwa na Mwamba uliopigwa; walipokuwa wagonjwa, Yeye alikuwa na nyoka wa shaba kwa ajili ya upatanisho kwa ajili ya ugonjwa wao. Na loo, jinsi ilivyokuwa ni ajabu!

²⁶ “Lakini,” akasema, “Mpenzi, ninaamini aliharibu kitu hicho chote aliposema, ‘Lakini, ole, Yehova hafanyi hivyo tena. Kwa namna moja ama nyingine sikuzote nimeamini ya kwamba—ya kwamba Yehova daima hudumu yeye yule, Yeye—Yeye kamwe hawezi kushindwa. Nami ninaamini ya kwamba sababu ya sisi, kuishi katika siku tunazoishi, ni kwa sababu watu wetu wamepoteza imani kwa Yehova.

²⁷ “Ninaamini ya kwamba Yeye hapatikani na mauti, wala hazeeki na kufifia, ananinii tu, kwa urahisi, ni Yehova yeye yule, Naye anatutarajia tusininii... Sidhani ya kwamba ningemdharau au kutomheshimu huyo mheshiwa rabi, lakini wakati aliposema asubuhi ya leo katika ujumbe wake ya kwamba Yehova hakufanya miujiza tena, kwamba jambo pekee alilotaka tufanye lilikuwa ni kuja kanisani, na kutoa zaka zetu, kuishi maisha mazuri tuwezavyo, Naye angetupeleka Nyumbani Utukufuni, ni—ni vigumu kwangu kuamini hilo, Mariamu. Ni—ninaamini ya kwamba Yehova anatutaka tutembe pamoja Naye kama walivyofanya katika siku hiyo.”

Ndipo basi hapana shaka ikawa kwamba Mariamu alisema, “Loo, Mpenzi, unajua...? Tunapaswa kusoma Maandiko kwanza.”

²⁸ Vema, kama umewahi kuwa katika nyumba ya Wapalestina na kuona baadhi ya maskini zile alama za kale, vitabu vya Biblia viliwekwa katika, kama ninii, linaitwa *gombo*, limefingirishwa kwenye, kama fimbo, nao waliyaweka kwenye chombo kama kikapu cha takataka, na kuyasukumia tu kwenye chombo hiki. Na, kama vile Gombo la Isaya, Gombo la Yeremia, na manabii hao wote yalivyokuwa mle ndani, na kwa hiyo haikuleta tofauti yoyote walisoma Gani, kwa sababu walijua yote yaliamriwa na Mungu, kwa sababu walikuwa ni manabii wao.

Kwa hiyo Yusufu akasema, “Vema, mpenzi wangu, wa—waweza kuingia ndani ulete moja ya hayo Magombo?”

Kwa bahati tu aliingiza mkono akashika hilo Gombo na kulitoa, akasema, “Vema, Mpenzi, leo inaonekana kana kwamba tutasoma kutoka katika Kitabu cha Isaya.”

²⁹ Kwa hiyo akafungua hilo Gombo, naye Yusufu akaanza kusoma, nayo akili yake...macho yake yakaangukia sehemu hii: “Bikira atachukua mimba, naye atamzaa Mwana. Nao watamwita Jina Lake Mshauri, Mungu Mwenye Nguvu, Mfalme wa Amani, Baba wa milele.”

³⁰ Basi alipofika mwisho, maskini msichana huyo bikira aliyeketi karibu naye, akasema, “Hebu kidogo, Yusufu, Mpenzi. Nabii anamaanisha nini na bikira kuchukua mimba?”

³¹ Vema, huenda Yusufu alisema hivi: “Mpenzi, hilo kidogo ni la kilindi sana kwangu. Silielewi, bali ninaliamini. Ni vile tu Biblia ilivyosema. Sijui jinsi litakavyotukia kamwe, bali tunajua hili, Mpenzi, tunajua ya kwamba Isaya alikuwa nabii wa Yehova, kwa hiyo akiwa na upako wa Roho Mtakatifu wa Mungu juu yake, asingeweza kutabiri uongo, kwa sababu alizaliwa nabii, nasi tunajua ya kwamba Maneno yake ni ya kweli. Basi aliposema, ‘Bikira atachukua mimba,’ huyo hakuwa Isaya, huyo alikuwa ni Yehova wetu, naye Yehova anaweza kufanya lolote ambalo anasema atafanya.”

³² Basi walipokuwa wakinena habari zake, na kuendelea, jinsi Jina Lake lingelitwa Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele, na uwezo wa kifalme utakuwa mabegani Mwake wala Ufalme Wake hautakuwa na mwisho, na kadhalika, yeye alisema, “Hapana shaka ni Mtu yule yule ambaye nabii Musa alituahidia, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi,’ kwa hiyo hana budi kuwa ni Masihi.”

³³ Yusufu akasema, “Ninaamini waandishi wanalifasiri hivyo, ya kwamba huyu atakuwa ndiye Masihi ajaye.” Basi jioni ilipopita, ibada ya usiku ikakaribia, mbona, wakarudi kanisani tena.

³⁴ Basi ilikuwa ni kesho yake asubuhi alipokuwa akienda kuteka maji, angeweza kusikia nyundo njiani, ambapo msumeno, ambapo Yusufu alikuwa akijenga nyumba yao. Ndipo alipoamka, na kula kiamshakinywa chake, akauchomeka mtungi mdogo chini ya mkono wake, akaanza kushuka kwenda kwenye kisima cha umma mjini. Sasa, kama tungalikuwa na wakati ningetaka kukaa kwenye kisima hicho kwa muda, bali hatuna wakati.

³⁵ Kwa hiyo alipokuwa akienda huku ameinamisha kichwa chake, akitafakari, asingeweza kuliondoa moyoni mwake, ndipo akasema, “Tamshi hilo ambalo Yusufu aliniambia nilipomsimamisha kwenye Andiko hilo la Isaya 9:6, na jinsi ambavyo yeye—yeye aliniambia, ‘Mpenzi, unajua, nafikiri wewe, daima niliwazia, ulikuwa ndiye mwanamke mrembo kuliko wote niliyepata kumwona, lakini kwa namna fulani katika dakika chache zilizopita, umekuwa mrembo zaidi kuliko hapo awali, macho yako makubwa ya hudhurungi yanametameta, na wakati

tu tulipotaja Maandiko haya. Kwani yalikusisimua sana? Ama ilikuwaje?” vema,” akashangaa, “ni kitu gani hapo aliposema, Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana? Nashangaa ni kitu gani kilichonifanya nijisikie jinsi nilivyojisikia?”

³⁶ Na papo hapo, maskini msichana huyo alipokuwa akitembea, aliona kitu kikimemetesha, naye akaangalia kote na, “Hapana shaka ilikuwa ni jua,” akasema, “ambalo liliangazia mwamba juu ya kilima cha jangwani kule, mahali fulani.” Basi alipokuwa akienda zake, akiwazia juu ya yale yaliyokuwa yakitukia, na yale waliyokuwa wakizungumzia, alikata kona inayoelekea kwenye kisima cha mjini, ambapo kina mama wanakutana huko nje asubuhi na mapema kushusha ndoo zao, ama wao . . . mitungi yao, zaidi ni kama mtungi au jagi.

³⁷ Ina shingo ndefu, mikono miwili, walikuwa na kulabu waliyoitia chini yake, na winchi, wakashusha jagi, kwa kuwa limetengenezwa kwa udongo, mbona, likazama. Wangeyavuta maji juu tena kisha wajitwike vichwani mwao, na kurudi moja kwa moja nyumbani, na labda lina galoni tano au sita za maji, ya kutosha kwa siku, isipokuwa walikuwa wanafua, ndipo basi, kwa kawaida, walienda mahali pa kufulia.

³⁸ Sasa, alipokuwa akipiga kona, aliiona Nuru hiyo ikimemetesha tena. Naye alipoangalia, ilipombidi kupitia mahali padogo, pembamba, ambapo mtu mmoja tu angeweza kupitia, huyo hapo Gabrieli amesimama, yule Malaika Mkuu. Haikuwa ni jua, j-u-a, aliloona likiakisi, alikuwa akimfuata, naye akakutana naye, ambapo alimfikisha mahali ambapo ingembidi kumwangelia. Basi akaangalia, naye alikuwa amezungukwa na mwangaza mtupu wa Nuru. Ikamtisha maskini yule bikira, na hapana shaka akaunyakua mtungi wake wa maji, nayo hayo macho makubwa yakakodolewa, yakamwangelia huyo Malaika Mkuu.

³⁹ Akasema, “Salamu, Mariamu,” ama *simama*, “umepewa neema tele mbele za Mungu.” Loo, napenda hilo. Maskini mwanamke huyo katika jiji duni sana lililokuwako ulimwenguni wakati huo, unaojulikana, mji katili sana, kwa vyovyote vile, katika Palestina. Na mle ndani alikuwa ameishi maisha mazuri sana mpaka Mungu akamchagua kwa ajili ya kazi fulani ambayo Yeye alikuwa anaenda kuifanya. Hapo akautazama uso Wake, nao ukamshtua.

⁴⁰ Mwajua, kwa kawaida ni wakati tunapowazia juu ya mambo hayo . . . Biblia ilisema, “Kukiwapo sifa nzuri yoyote, ukiwapo wema wowote, yatafakarini hayo.” Nafikiri sababu ya kutokuona zaidi ya yale tunayoona, tumeweka nia zetu kwenye mambo mengine mengi kupita kiasi. Nafikiri Malaika bado wangetutokea kama tungaliweka tu nia zetu juu yao, lakini tunawazia juu ya jambo lingine, kule tunakoelekea, kipindi fulani tunachopaswa kuangalia, ama—ama ununuzi fulani

tunaopaswa kufanya. Lakini Maandiko yetu yanatwambia, “Utafutuni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake, na hayo mengine yote mtaongezewa.”

Na hapo basi tunapoona jambo hilo, kwamba Yeye alisema, “Wewe umepewa neema tele mbele za Mungu.”

⁴¹ Nasi tunaona tena, sitaki kuacha Andiko hili, lakini ilikuwa ni Kleopa na rafiki yake wakienda zao Emau, walipokuwa wakienda kule, wamevunjika mioyo, wakinena juu ya Yesu kusulubiwa na kufa, na zile hadithi walizokuwa wamesikia kuhusu Yeye kufufuka katika wafu, nao hawakuziamini. Barabarani wakienda, wakirudi, labda, kwenda kazini Jumatatu asubuhi, walipokuwa njiani wakirudi, ilikuwa ni wakati walipokuwa wakimwazia Yeye ndipo alipowatokea, akatokea vichakani, na kuanza kuzungumza nao, kama tu mtu wa kawaida.

Akasema, “Loo, mbona mmefadhaika sana? Mna shida gani?”

Wakasema, “Kwani wewe ni mgeni tu hapa?”

⁴² Mnaamini sasa, hili kidogo ni ngumu, lakini watu waliokuwa wametembea pamoja Naye, na kuzungumza Naye, na kutembea pamoja Naye siku nzima baada ya kufufuka Kwake, Yesu yeye yule, wala hawakumjua? Yeye—Yeye atajifunua Mwenyewe kwa yeyote atakayejifunulia. Loo, ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba Yeye ataondoa vivuli kutoka kwa kila moja ya macho yetu, naye ataingia katika jengo hili na kujifunua Mwenyewe katika nguvu za kufufuka Kwake, ili kila mtu apate kumwona, mwenye dhambi, kama Mwokozi wao; wagonjwa, kama Mponyaji wao.

⁴³ Nasi tunaona ya kwamba alitembea pamoja nao siku nzima, halafu basi akajifanya kana kwamba alikuwa akienda mahali pengine, ama akipita, nao wakamshawishi aingie ndani. Loo, napenda hilo, kumshawishi aingie ndani, “Loo, Yesu, Wewe—Wewe—Wewe uko hapa kanisani, usiku wa leo, Huna budi kwenda nyumbani pamoja nami! Ninataka kukupeleka nyumbani kwangu. Sitaki kamwe kupoteza hisia hii ya Uwepo Wako. Hebu nikupeleke nyumbani, nawe uingie ndani ukae pamoja nami.” Kamwe sitaki kupoteza hisia hiyo. Hilo si lingekuwa ni zuri sana?

⁴⁴ Mwajua, ninataka kusimama hapa katika ujumbe wangu kwa muda kidogo tu, na kusema mambo matukufu sana niliyowahi kuona yakitendeka ni wakati *Kitu fulani* kiliponitia mafuta. Laiti ningaliweza kukaa mahali hapo wakati wote.

⁴⁵ Mlisoma katika kitabu, usiku ule wakati yule mwendawazimu alipokimbia jukwaani huko juu apate kuniua huko . . . Ilikuwa wapi . . . ? Portland. Ulikuwa huko, Ndugu Jack, ama ilikuwa, Ndugu Brown alikuwepo, wakati mwendawazimu yule alipotoka mbio akaniue, na kutishia kufanya hivyo, jamaa

mkubwa mno, pandikizi la mtu. Na badala ya kumchukia mtu huyo, nikampenda. Asingefanya hivyo, labda alikuwa ni mtu mwenye familia, kama nilivyokuwa nayo, naye asingefanya hivyo, ni ibilisi juu yake aliyekuwa akifanya hivyo. Ndipo nilipompenda, sikumwogopa basi. Upendo hutupilia nje hofu, ni wakati unapoweza kupenda.

⁴⁶ Mlisikia hadithi kuhusu maskini mama oposamu akija nyumbani, upendo, inahitaji upendo kushinda.

⁴⁷ Wakati yule fahali alipokuwa akitaka kuniua huko nje kondeni, akanikimbilia moja kwa moja, na si kwamba nilimchukia. Nilikuwa mlinzi wa wanyama pori, nikanyosha mkono kuchukua bunduki, nami nilikuwa nimeiacha kwenye gari langu, ndipo nikafurahi niliacha, baadaye. Akaja mbio, nami nikawazia, “Vema, kama itanibidi kufa, afadhali nife nikimkabili, siwezi kumtoroka, hakuna kitu, nipate kuondoka njiani.” Ndipo papo hapo nikawaza, “Vema, kama itanibidi kwenda, ninataka kwenda nikimtaazama.”

⁴⁸ Basi nilipofanya hivyo, akanikimbilia moja kwa moja, maana angenishika, kwa vyovyote vile. Naye alikuwa na mnyororo ulioning’inia kutoka puani mwake. Ndio kwanza amwue mtu mweusi, majuma machache kabla ya hapo. Nilisahau kuhusu yeye kuwa kwenye eneo hilo, nilikuwa niende huko kumwombea mgonjwa. Akatupa goti lake chini namna *hii* na kutifua vumbi, akanguruma, naye huyu hapa anakuja. Nami sijui ni kwa nini, lakini *jambo fulani* lilitukia.

⁴⁹ Daima uponyaji unapotukia, ama chochote kile, kuna *jambo fulani* linalotukia. Upendo unaingia, huo, nao unaondoa tu kila kitu njiani. Loo, nakwambia, ndugu, unaweza kuwa na theolojia yote unayotaka, lakini nipe upendo kila wakati.

Tangu kwa imani nilipokiona kijito kile,
Kinachosababishwa na kububujika kwa
majeraha yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo
wangu,
Na utakuwa hata nitakapokufa.

⁵⁰ Upendo! Loo, laiti ningaliishi katika mazingira hayo wakati wote!

⁵¹ Basi *huo* uliponigusa, nikasema, “Kiumbe cha Mungu, mimi ni mtumishi wa Mungu. Niko njiani kwenda kumwombea mmoja wa watoto Wake wagonjwa. Sasa, niko katika eneo lako, niko katika uwanja wako hapa, Sikutaka kukusumbua, lakini katika Jina la Yesu Kristo, rudi ukalale chini, sitakusumbua.”

⁵² Naye alionekana kana kwamba alikuwa anaendelea kuja. Huyu hapa anakuja, upesi tu alivyoweza. Nilisimama tu kimya, bila hofu kuliko nilivyo nayo sasa hivi. Ndipo alipofika yapata futi tatu kutoka kwangu, akasimama, akaniangalia, alionekana amedhoofika sana, upande mmoja kisha mwingine, akageuka,

akaenda kule, akalala chini. Nikapita karibu naye umbali wa futi mbili, nikatembea moja kwa moja karibu naye. Upendo hushinda. *Jambo fulani* hutukia, *jambo fulani* hutukia.

⁵³ Hivi majuzi usiku nilikuwa nikiwaambia kuhusu huko Mexico wakati Ndugu Jack alipokuwa kule. Kulikuwako na mzee mmoja wa Kimeksiko aliyekuja jukwaani, alikuwa kipofu kabisa, na maskini jamaa huyo mzee, ninii yake. . . Uchumi wao una uwiano mbaya sana nao hawana chakula. Jamaa huyu mzee hakuwa na viatu vyovyote, na kofia kuukuu mkononi mwake, iliyoshonwa kwa kamba, na amevaa koti kuukuu, lililochakaa, na suruali karibu kufikia magotini mwake, na imejaa mavumbi. Alikuwa akitembea jukwaani ameshika rozari ndogo mkononi mwake, lundo dogo la shanga, naye akanijia, akisema jambo fulani, mtu fulani alikuwa akimwongoza. Nami nikasimama na kumtazama.

⁵⁴ Nakwambia, ndugu, mpaka unapoweza kuhisi hali ya mtu mwingine, kamwe huwezi kumsaidia. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu Mungu aliupenda sana ulimwengu, alihurumia.

⁵⁵ Basi nikamwangalia, nikawazia, “Huyo hapo, labda kundi la watoto wadogo mahali fulani, huku wakifanya kazi ya peso chache kwa siku. Na sasa baada ya haya yote, labda pengine. . . kamwe hajapata mlo mzuri maishani mwake, naye huyu hapa katika hali hiyo. Sasa maumbile yamekuwa mabaya sana kwake, ama majaliwa yake yamempofusha.” Naye alikuwa. . .

⁵⁶ Nikaweka mguu wangu kando ya wake, nikawaza, “Mimi huyu hapa nimesimama nimevaa suti nzuri na jozi ya viatu, jozi nzuri ya viatu, nami sijui kama aliwahi kuvaa jozi ya viatu maishani mwake.” Nikawaza, “Hilo si sawa. Nina jozi nyumbani, nina suti nyingine nyumbani, mtu huyo ana haki kwazo kama tu nilivyo nayo mimi.” Nikaweka mguu wangu kando ya wake, nikawazia ningempa viatu vyangu kabla sijasema lolote. Mbona, mguu wake ulikuwa mkubwa zaidi, na ma—mabega yake, mapana zaidi, nisingeweza kumpa koti langu. Nikawaza, “Mungu, nimfanyie nini?” Kama baba yangu mzee angeishi, angekuwa karibu umri wake.

⁵⁷ Ilikuwa ni kitu gani? Kuingia ndani. Mara jambo fulani likatukia. Nikaanza kuhisi uwepo huo wa upendo, huruma kwa huyo mzee.

Akanyakua shanga ndogo, akaanza kupiga makelele, “Salamu, Mariamu, mama wa Mungu, bariiki. . .”

Nikasema, “Hizo hazihitajiki. Ziweke tu kando.”

Naye akamwambia Ndugu Espinosa, “Yuko wapi mponyaji? Ninataka kumshika.”

⁵⁸ Na—nami nikasema, “Mwambie tu ainamishe kichwa chake.” Nikamkumbatia huyo mzee, nikaanza, nikasema, “Bwana Yesu, maskini mzee huyu, siwezi kumpa viatu vyangu,

hawezi kuvivaa, siwezi kumpa koti langu, lakini, Bwana Mungu, Wewe Ndiwe wa pekee unayeweza kumsaidia sasa, unaweza kumpa kitu ambacho kitamfaa, hicho ni kuona, huko ndiko anakotamani sana.”

⁵⁹ Na mara niliposema hivyo, nikasikia mtu fulani akipiga makelele, “Gloria a Dios!” Naye huyo hapo, angeweza kuona vizuri kama nilivyoweza mimi, akikimbia jukwaani upesi tu alivyoweza kwenda.

⁶⁰ Basi kesho yake usiku kulikuwa na lundo la nguo, skafu kuukuu, na aproni, na makoti machakavu, na matambara, na kofia zimelundikwa pale, mara mbili ama tatu urefu wa *hii* hapa, na juu *hivyo*. Jinsi nilivyowahi... Jinsi walivyowahi kupata kilicho sahihi, sijui. Lakini nini? Waliona kitu fulani. Loo, *jambo fulani* linapotukia, jambo fulani linatukia!

⁶¹ Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Mariamu asubuhi ile, hapana shaka jambo fulani lilitukia wakati alipokuwa akiwazia juu Yake, na hapo akatokea mbele zake. Lilikuwa ni jambo lile lile kwa Musa kama ilivyokuwa kwa Mariamu. Yeye alisema, “Utachukua mimba tumboni mwako, na kuzaa mtoto.”

⁶² Sasa, alijua ujumbe wa Malaika ulikuwa wa Kimaandiko. Sijali alikuwa ni malaika wa aina gani aliyetokea, kama ujumbe wa malaika huyo si wa Kimaandiko na ahadi ya Mungu, achana nao. Kumekuwa na kutokea kwa malaika wa kila namna, kila kitu, nao wanaleta jumbe za kila namna. Kama Malaika wa Bwana, ambaye mimi ni mtumishi wake, angekuja, kama malaika huyo angekuja, haidhuru alionekana kama Nguzo ya Moto jinsi gani, jinsi alivyoonekana kama Nuru, kama ujumbe wake haukushuhudia Neno hili, ningeachana naye na kumwacha alaaniwe, haina budi kuwa katika *Hili*. Joseph Smith, mwajua, alimwona malaika, alisema, bali hakushuhudiwa na Neno.

⁶³ Naye Mariamu alijua ya kwamba, alikuwa ndiyo kwanza asome siku iliyotangulia, Isaya 9:6, ya kwamba jambo fulani lilikuwa karibu kutukia. Naye alijua lilikuwa njiani wakati huo.

⁶⁴ Musa, vivyo hivyo, alipokuwa ameikatia tamaa theolojia yake, naye alikuwa upande wa nyuma ya jangwa, akiwachunga kondoo wa Yethro, basi siku moja aliona M—Mpira wa Moto ukiwa kwenye kichaka huko nyuma, naye akaja na kuvua viatu vyake kama alivyoagizwa, naye akasikiliza aone ilikuwa ni kitu gani. Lakini alipoona Malaika huyo alikuwa wa Kimaandiko, kasema, “Nimesikia vilio vya watu Wangu nami nimelikumbuka agano Langu,” alijua ya kwamba Mungu alifanya ahadi, na ilikuwa... huyo alikuwa ndiye Malaika ambaye angeambatana naye.

⁶⁵ “Ninakumbuka ahadi Yangu na agano Langu. Nimeona mateso ya watu Wangu, nami nimeshuka kuja kuwakomboa.” Musa alijua haikuwa yake tena, kwa sababu ya hayo “*Mimi* nimeshuka kuja kuwakomboa.” Loo, hiyo ndiyo sehemu nzuri.

“*Mimi* nimeshuka. Wewe uwe tu msemaji Wangu.” Kwa hiyo akaona lilikuwa ni la Kimaandiko kabisa.

⁶⁶ Naye Mariamu aliona lilikuwa ni la Kimaandiko kabisa, kwa kuwa siku moja kabla alikuwa akilisoma, labda, katika Gombo, kama mchezo wetu mdogo wa kuigiza unavyoenda. Ninawaambia, ina faida kusoma Neno la Mungu, kila siku sasa. Yesu alisema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia *Mimi*.”

⁶⁷ Kwa maneno mengine, Yeye alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu,” ambazo zilipaswa kufanywa wakati Yeye atakapokuja, “basi msiniamini *Mimi*, bali nikizitenda hizo kazi, ijapokuwa hamniamini *Mimi*, aminini hizo kazi, kwa sababu hizo ndizo zilizotumwa na Mungu.”

⁶⁸ Tunamtazamia mgeni wa Mbinguni katika siku hii; ni ahadi ya Mungu. Vaeni haraka kuwaza kwenu kwa kiroho kwenye kilindi, enyi kanisa, pia kumbukeni, sasa tunamtazamia mgeni, na kuna wengi wanaodai jambo hilo. Lakini njia pekee ambayo tutamjua mgeni huyu wa Mbinguni, kwa sababu yeye atalishuhudia Neno. Hiyo ni kweli kabisa.

⁶⁹ Alijua ya kwamba Malaika huyo alitoka kwa Mungu wakati alipoona tendo Lake. Akamwangukia, hapana shaka ni Malaika. Akasema, “*Mimi* ni Gabrieli, ninayesimama mkono wa kuume wa Mungu.” Sasa, Mungu anapokuwa tayari kufanya jambo fulani, Yeye humtuma mjumbe, daima. Daima amefanya hivyo, daima atafanya hivyo. Gabrieli alitangaza kule Kuja mara ya kwanza kwa Kristo, Gabrieli atatangaza Kuja mara ya pili kwa Kristo. Hiyo ni kweli. Jambo fulani kuu liko karibu kutukia.

⁷⁰ Nasi tunaona Malaika huyu, wakati aliposema “Salamu, Mariamu,” na kumwambia yale yatakayotukia, yeye hakumtilia shaka, kwa sababu alijua alikuwa wa Kimaandiko kabisa, kwamba ilipaswa kuwa hivyo.

⁷¹ Sasa, tunamtazamia mjumbe katika siku hizi za mwisho, kwa sababu Yesu alisema itakuwa, kwa sababu manabii wote walisema itakuwa, Malaki alisema itakuwa, manabii wote wameshuhudia. Yesu katika kivuli chenyewe cha msalaba alinena zaidi juu ya Kuja Kwake mara ya pili kuliko alivyonena juu ya kuondoka Kwake. Basi tunapona mambo haya yakianza kutimia, afadhali tuanze kuyachunguza Maandiko, kwa sababu Yeye alisema watatokea Makristo wa uongo na manabii wa uongo, nao wangeonyesha ishara na maajabu, hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini.

⁷² Billy Graham alisema katika ujumbe mmoja, hapa majuma machache yaliyopita, “Tayari imewapoteza walio Wateule.” Sikubaliani na huyo mwinjilisti, haiwezi kuwapoteza walio Wateule, kwa sababu wameteuliwa na Mungu.

⁷³ Yesu alinena kwamba katika siku zile kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu, ingekuwa kama ilivyokuwa katika Sodoma. Na kama tulivyolichukua hapo awali, mwisho... hili, katika juma hili, kwamba kulikuwa na Malaika aliyekuja Sodoma, wakiwa watatu, kwa matabaka matatu ya watu. Mojawapo lilikuwa ni Wasodoma, hilo lingine lilikuwa ni kanisa vuguvugu, hilo lingine lilikuwa Kanisa teule na lililoitwa litoke; Ibrahimu na kundi lake, Lutu na kundi lake, na Sodoma na kundi lao. Wote...

⁷⁴ Wawili wao walishuka, hao wainjilisti walishuka kwenda kuihubiria Sodoma, na, kulitoa kundi hilo la watu, la waaminio, kule chini, aliwatoa wachache tu.

⁷⁵ Lakini tunaona, ya kwamba Yule aliyebaki nyuma kwa Kanisa teule, Yeye alionyesha ishara. Na ilikuwa ni Mungu akifanya hivyo, haikuwa hadithi ya uongo, haikuwa thiofania, thiofania haili. Alikula nyama ya ndama, na kula mkate wa mahindi, ugali wa mahindi, na siagi juu yake, na kunywa maziwa kutoka kwa ng'ombe. Thiofania haili wala kunywa, ilikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Ndivyo hakika.

⁷⁶ Naye alikuwa akizungumzia nini? Yesu alisema, "Kama katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa," Mungu atakuja tena, aje katika mwili wa watu Wake ambao amewanunua na kuwatakasaa, naye atalionyesha Kanisa Lake teule ishara ile ile aliionyesha Kanisa Lake teule huko nyuma.

⁷⁷ Hakukuwa na, "Tokeni kwake," hakukuwako na *hili, lile*, alikuwa tayari ametoka kwake, Ibrahimu alikuwa ametoka. Lakini wale malaika wengine walikuwa wakiita, wakiita huko chini, lakini Ibrahimu alikuwa tayari ametoka. Nalo Kanisa, neno lenyewe *kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke," Kanisa la Mungu tayari limeitwa litoke, limeitwa litoke.

⁷⁸ Naye alimpa ishara ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye. Na alipofanya hivyo, huku amegeuza mgongo Wake, Yeye alisema (Sara alikuwa hemani nyuma Yake, akicheka.), kwa nguvu fulani, jambo lile lile ambalo Yesu alidhihirisha katika kuja Kwake, lilidhihirishiwa Msamaria na Myahudi pia, na imebashiriwa ya kwamba katika siku hizi za mwisho ya kwamba Yeye angemtuma Mjumbe Wake tena. Naye Mjumbe huyo usiku wa leo si mwanadamu, la bwana, ni Roho Mtakatifu, huyo ndiye Mjumbe Wake. Mungu katika Kanisa Lake, akitenda kazi, akionyesha ishara na maajabu kabla tu ya kuonekana Kwake.

⁷⁹ Sasa, kumbukeni, Malaika huyu hana budi kuwa ni Malaika wa Kimaandiko. Isitoshe, tumeonywa na Mungu kuhusu manabii wa uongo, Biblia ilisema, "Akiwapo mtu miongoni mwenu anayejiona kuwa ni nabii," ama kadhalika, "na yale asemayo hayatimii, basi msimwogope, mimi siko pamoja naye. Lakini yale asemayo yakitimia, basi niko pamoja na nabii huyo, msikieni." Hiyoyi ni kweli.

⁸⁰ Kwa hiyo, tunaona leo ya kwamba ujumbe huo ni ujumbe wa kweli wa Biblia. Ni kurudi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudi kwenye nguvu za Mungu, kurudi kwenye Pentekoste tena, kuirudisha mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, ama, ya watoto iwarudie baba zao, hasa, katika siku hizi za mwisho. Tunamtazamia Mjumbe wa Mbinguni, nami ninaamini Yeye yupo hapa usiku wa leo. Amina. Ninaamini ya kwamba Yeye yupo hapa. Yeye hufanya nini? Hushuhudia.

⁸¹ Sasa sikilizeni, enyi marafiki, usichukue kabadala, usipeane tu mkono na mtu, na kuandika jina lako kwenye kitabu. Hilo ni—hilo ni—hilo ni—hilo ni, kadiri linavyoenda, hilo ni sawa. Huenda nikaninii . . . Huenda ikakusaidia kutoka kwenye baa, na kuingia mahali pa heshima, na kujaribu kuishi vizuri, hilo halitalitua hata hivyo, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu.”

⁸² Sasa, *kuona* maana yake, “kufahamu.” Kuna watu wengi sana wanaosema wamezaliwa mara ya pili, wala hawawezi kuufahamu Ujumbe wa Mungu, hawawezi kumwona Malaika wa Bwana, macho yao yamepofushwa, ndugu, mtu asipozaliwa kwa Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu yeye yule aliyeliandika Neno atalithibitisha hilo Neno, na uthibitisho ule ule wa Roho Mtakatifu ndani yako. Mnaona ninalomaanisha? Litajishuhudia Lenyewe.

⁸³ Ndipo roho yetu inashuhudia pamoja na Roho Wake, kwa sababu Roho Wake hushuhudia Neno Lake. “Neno la Mungu lina ukali, lina nguvu zaidi,” Waebrania 4, “kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, hata huchoma hata kugawanya mafuta yaliyomo ndani ya mfupa, tena ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo.” Hiyo ni kusema, BWANA ASEMA HIVI, Neno la Bwana, sawa kabisa, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, akitokea katika Kanisa Lake teule.

⁸⁴ Loo, tuna uamsho mkuu unaoenea kila mahali nchini, ukiita kutoka Sodoma, na kadhalika, bali katika Kanisa teule tuna Mtu huyo, Mungu, Mungu yeye yule aliyekuwa huko nyuma. Kuna Mmoja tu wao, na Huyo alikuwa katika Kanisa Lake akijidhihirisha Mwenyewe kuwa Bwana Yesu Kristo aliyefufuka, yeye yule jana, leo, na hata milele. La kimaandiko!

⁸⁵ Kama hakuwa pamoja na Maandiko, hakuyashuhudia Maandiko, hakulithibitisha Neno Lake, basi nisingemwamini, lakini kwa kuwa Yeye hufanya hivyo, basi ninajua ametoka kwa Mungu, kama tu Mariamu alivyofanya, amina, loo, kama Musa alivyofanya, ama yeyote wa hao wengine.

⁸⁶ Kama halikuwa la Kimaandiko, sasa, huko nyuma katika Agano la Kale walikuwa na zaidi ya njia moja ya kujua. Kama mtu aliota ndoto, ama nabii alitabiri, mnajua walifanya nini na hiyo? Waliwapeleka mbele ya Urimu na Thumimu zilizotundikwa kwenye nguzo. Inaaminiwa Urimu na Thumimu

ilikuwa ni yale mawe kumi na mawili ya kuzaliwa katika ninii cha Haruni. . . , ama, kifuko chake cha kifuani, kilichobeba jiwe la kuzaliwa la kila mmoja.

⁸⁷ Ndipo akakitundika kwenye nguzo, na kama nabii alisimama na kutabiri, na haidhuru lilisikika halisi jinsi gani, kama ya kimbinguni hayakujibu tena, mkusanyiko wa Nuru za upinde wa mvua pande zote, nazo hizi zikimetameta namna *hiyo*, haidhuru nabii alisema nini, alikuwa amekosea; haidhuru huyo mwotaji aliota nini, ilikuwa ni makosa. Lakini Mungu daima hujibu kwa njia ya kimbinguni. Amina.

⁸⁸ Sasa, nao ukuhani huo ukaisha, na Urimu na Thumimu zikaondolewa, lakini Mungu ana Urimu na Thumimu nyingine, *Hii* ndiyo. Neno la Mungu ni Urimu na Thumimu, hilo ni Neno la Mungu. “Neno la kila mtu na liwe uongo na Langu liwe kweli,” alisema Mungu. “Mbingu na nchi zitapita,” alisema Yesu, “bali Neno Langu halitapita kamwe.”

⁸⁹ Sasa, basi kama mmoja akinena wala si la Kimaandiko, msiamini. Kama akinena na ni la Kimaandiko, ngoja kidogo, lijaribu kwa Urimu na Thumimu, basi kama ya kimbinguni yakijibu tena kwamba ni kweli, basi liamini. Hiyo ndiyo njia ya kuamini Ujumbe wa kweli. Kama Biblia ikiahidi chochote na Biblia inasema ndivyo kilivyo, hiyo ni Urimu na Thumimu ya Mungu, kama mhubiri akihubiri, akihubiri, kama Biblia ilivyosema, huyo ni mjumbe wa Mungu, shahidi wa Mungu, basi kama ndiye, basi mambo ya kimbinguni ya Neno hilo yatadhihirishwa na kuthibitika kwamba ni Mungu. Mungu hutimiza ahadi Yake.

⁹⁰ Tunamtazamia Mjumbe, Mjumbe huyo ni Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena,” Yesu alisema, “hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Sasa, neno hilo hapo *zaidi*, katika tafsiri sahihi, ninalitumia pale, “na nyingi zaidi,” kwa sababu ilisema katika toleo la King James *kuu zaidi*. Ni nani angeweza kufanya makuu zaidi? Aliwafufua wafu, akasimamisha maumbile, akafanya kila kitu.

⁹¹ Lakini wakati huo Yeye alikuwa katika Mtu mmoja, Mungu wote alifichwa ndani ya Mtu mmoja, Yesu Kristo, lakini katika wakati huu Yeye yuko kote ulimwenguni katika Kanisa Lake, akifanya nyingi zaidi, kazi zile zile. “Kazi zile zile nizifanyazo wao nao watazifanya, nyingi kuliko hizi nitazifanya, kwa sababu ninarudi kwenye Nguzo ya Moto niliyokuwa kabla sijafanyika mwili na kukaa duniani. nilijionyesha Mwenyewe kuwa hai kwa kazi zile zile na madhihirisho yale yale niliyofanya.” Hiyo ni kweli kabisa. Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa duniani,

“Nimetoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu.” Hiyo ni kweli? Vema.

⁹² Kama alikuwa ni Mungu, alizungumziwa kule siku moja, nao walikuwa wakisema Naye kuhusu kutokuwa na umri wa miaka hamsini bado na ati alimwona Ibrahimu, Yeye akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” *MIMI NIKO* alikuwa ile Nguzo ya Moto iliyokuwa kwenye kichaka pamoja na Musa, hiyo ilikuwa ni Nguzo ya Moto ya Kimaandiko. Yuyo huyo ndiye MIMI NIKO, sio “Nilikuwako,” au “nitakuwako.” “Daima MIMI NIKO yeye yule tu jana, leo, na hata milele.”

⁹³ Tunaona wakati MIMI NIKO alipofanywa kuwepo miongoni mwetu katika Mwili wa Mwanaye Mwenyewe aliyemuumba, Mwili Wake Mwenyewe, akabadilisha kinyago chake kutoka kwa Mungu akawa mwanadamu, apate kuturudisha kwenye wokovu na kurudi kwenye bustani ya Edeni tena, akavuka Mwenyewe, akatandaza mahema Yake miongoni mwetu, na kula kama sisi, na kulala kama sisi, na kutembea kama sisi na kufanana nasi, Yeye alifanyika sisi, ili sisi kupitia Kwake tupate kufanyika Yeye, warithi pamoja Naye katika ule Ufalme.

⁹⁴ Ndipo, tunapoiona Nguzo hiyo ya Moto, wakati ilipokuwa pamoja Naye, ilifanya ishara na maajabu, Kisha akakiri, “Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo kazi. Kwa maana, amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, mpaka amwone Baba akilitenda, pia. Naye Mwana hufanya yale Baba anayomwonyesha. Yeye anatenda kazi, nami ninatenda kazi hata sasa.” Amina. Sawa.

⁹⁵ Alikufa, akafufuka tena siku ya tatu. Na siku chache baadaye kulikuwako na maskini Myahudi mkosoaji, mwenye pua iliyopinda, akiwa na lundo la vitu mfukoni mwake, akishuka kwenda kulitesa Kanisa, wote waliokuwa katika Njia hii. Akatoka kuninii, akienda zake Dameski, naye akabwagwa chini, naye alipoangalia juu, aliona Nguzo kuu ya Moto ikining’inia pale, ikisema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “U nani wewe, Bwana? Nguzo hii ya Moto ni nani?”

“Nalitoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu.” Akasema, “Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo.”

⁹⁶ Nabii alisema kutakuwa na mvua ya masika na mvua ya vuli. Na katika mvua ya vuli kungekuwako na mvua ya masika na ya vuli pamoja, Kanisa kuu, la kote ulimwenguni, ambao ungeenea kutoka upande mmoja wa ulimwengu hadi upande mwingine wa ulimwengu, Ujumbe mkuu, ishara kuu na maajabu, zingetimizwa na Kanisa hili. Danieli alisema watu wamjuao Mungu wao katika siku hiyo watafanya mambo makuu. Hapo ndipo hasa tunapoishi katika siku hii.

⁹⁷ Sasa, jicho la kimitambo la kamera linaonyesha juu yetu ya kwamba Nguzo hiyo ya Moto ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Sasa, haina budi kufanya mambo yale yale iliyofanya ilipokuwa ndani Yake, la sivyo si Nguzo ile ile ya Moto. Lakini kama ikifanya mambo yale yale, unawezaje kuitilia shaka? Ni la Kimaandiko.

⁹⁸ “Salamu, Mariamu, umebarikiwa miongoni mwa wanawake. Umepata neema kwa Mungu.” Loo, Kanisa, salamu, mmebarikiwa miongoni mwa watu, kwa sababu mmepata neema kwa Mungu. Mameamini kwa ajili ya Uzima wa Milele, naye Mungu amewapa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sawa. Mjumbe huyu atakuwa Mjumbe wa kweli wa Mungu, Roho Mtakatifu, ambaye ndiye Ujumbe wa Mungu.

⁹⁹ Angalieni, Mariamu, mara alipoona lilikuwa ni la Kimaandiko, hakusema, “Nitaenda huko nione kama Dk. Jones anasema ni kweli au la.” Hakupitia pale kuona kama Rabi Kabinski alidhani ilikuwa sahihi au la, kamwe hakuwa na uhusiano wowote nalo. Mnajua alichosema? Alisema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu sawasawa na neno lako.” Kwa kuwa alijua Neno hilo lilikuwa ni Neno la Mungu, Mjumbe huyo alikuwa Mjumbe wa Mungu, Malaika huyo alikuwa ni Malaika wa Mungu, kwa sababu alidumu na Neno la Mungu. Amina. “Tazama, mjakazi wa Bwana.” Kasema, “Itakuwaje?”

Yeye alisema, “Roho Mtakatifu atakutia uvuli, na Kitu hiki Kitakatifu kitakachozaliwa kwako kitaitwa Mwana wa Mungu.”

¹⁰⁰ Akasema, “Mimi hapa, sijui jinsi itakavyotukia, haileti tofauti yoyote, unasema ndivyo ilivyo, ni la Kimaandiko, ninaliamini, ninalikubali.” Akaanza moja kwa moja kumsifu Mungu, kabla hajahisi uhai, kabla hajahisi ishara yoyote ya chochote, hakutaka ishara tena, alikuwa na Neno Lake na hilo tu ndilo lililokuwa muhimu. Amina. Ninapenda hilo.

¹⁰¹ Musa, mara alipomshika Mungu na kuona lilikuwa ni la Kimaandiko, hapa alienda Misri.

¹⁰² Mara Mariamu alipomshika, yu—yule Malaika alipomshika, hasa, naye akamwona, na akajua ilikuwa ni Mungu, kwa sababu lilikuwa ni la Kimaandiko, aliamini neno lake na kwenda huku na huko akishuhudia juu ya kitu ambacho hata hakikuonyesha ushahidi mmoja wa kuwahi kuwako.

¹⁰³ Jambo lingine, alishuhudia jambo ambalo halikuwa limewahi kutukia hapo kabla. Loo, Bwana asifiwe! Alishuhudia jambo ambalo halikuwa limewahi kutukia kamwe, bikira hakuwa amewahi kuchukua mimba kamwe. Lakini alikuwa na neno la Malaika, naye huyo Malaika alikuwa ni wa Kimaandiko, kwa hiyo alijua ilikuwa imeahidiwa. Naye Malaika alikuwa na Neno la Bwana na akaliahidi. Na kwa sababu alijiona kuwa

mnyenyekevu na duni, hata hivyo Mungu alikuwa amemchagua, kwa hiyo alifurahia tu jambo hilo.

¹⁰⁴ Naye akaondoka na ujumbe wake, akimwambia kila mtu atapata mtoto kabla hata hajapata ishara ya kwanza ya mtoto. Hakungoja, na kusema, “Sasa ngoja, hebu nijisikie, nione kama ninajisikia vizuri zaidi au la.” La, la. Loo, Mungu, tupe Mariamu wengi zaidi!

¹⁰⁵ Beaumont na walimwengu wengine wanahitaji Mariamu wengi kama huyo, ambao wanaweza kuliadini Neno la Mungu na kuanza kushangilia kabla jambo lolote kutendeka. Vipi kuhusu ninyi wanawake kwenye viti vya magurudumu nanyi ndugu na dada hapa wenye ugonjwa wa moyo, na maradhi, na kila kitu, wakati Uwepo wa Bwana uko karibu sana? Jamani, jamani! Mnajua ni Neno la Bwana, Bwana lililiahidi.

¹⁰⁶ Unasema, “Ndugu Branham, laiti ungalishuka na kuniwekea mikono!” Hilo silo, tayari umeponywa kwa sababu “Alijeruhiwa kwa makosa yako, alichubuliwa kwa maovu yako, adhabu ya amani yako ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake wewe uliponywa.” Tayari ni wakati uliopita.

¹⁰⁷ Lipokee tu na uanze kushangilia. “Asante, Bwana, sasa ninaliona. Mungu abarikiwe, nimeponywa, sijali yale mtu mwingine yeyote asemayo ama jinsi ninavyojisikia, nimeponywa, kwa vyovyote vile.” Jambo ndilo hilo.

¹⁰⁸ Ujumbe wa Malaika, daima umekuwa hivyo, hivyo ndivyo Mungu anavyotaka. Ulifanya nini? Lile badiliko... Kwa kuliadini Neno la Mungu, kulibadilisha mwelekeo wote wa kawaida wa maisha kwake. Litakufanyia jambo lile lile, hakika litafanya. Litakuchukua wewe mwenye dhambi, na kukuosha mweupe kama theluji. Litakuchukua wewe, mkosoaji, na kukufanya mmoja wetu, hakika litakufanya. Litakuchukua wewe uliye mgonjwa na kukupa afya. Litakuchukua wewe unayeenda zako kuzimuni na kukubadilisha, kukuelekeza juu Mbinguni. Liadini tu Neno Lake, na uliadini, na uanze kushangilia.

¹⁰⁹ Mjumbe wa Bwana yupo hapa, Roho Mtakatifu, akizunguka-zunguka juu ya watu, akiwatia mafuta. Kama wewe ni mgeni, unataka kujua watu hao wana shida gani, hivyo ndivyo ilivyo. Yoeli aliliahidi. Kwenye Siku ya Pentekoste Petro alisema, “*Hili ni Lile.*” Ninataka kuongezea kitu kwenye hilo: Iwapo *Hili* si *Lile*, ninataka kuweka *Hili* mpaka *Lile* litakapokuja, kwa sababu nina wakati mzuri sana na *Hili*. Nami ninaamini *Hili* ni *Lile*, *Lile* lile lililokuwa *Lile* kwenye Siku ile. Loo, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹¹⁰ Mariamu hakungojea, hakuwajali wakosoaji, hakuajali yale mtu yeyote aliyosema, alikuwa amekutana na Malaika. Aliona Sauti Yake, ama, aliuona Uwepo Wake, naye alijua ya kwamba alimwambia ukweli kwa sababu lilikuwa ni la

Kimaandiko, aliahidi baraka kwake, endelea tu, amini, naye alijua litatendeka. Loo, yeye . . . Kuna jambo fulani kuhusu hilo, unapogusa kitu kama hicho huwezi kutulia kukihusu.

¹¹¹ Malaika alimwambia ya kwamba binamu yake Elisabeti, aliyekuwa huko juu katika nchi yenye milima ya Yuda, alikuwa mkongwe, yapata umri wa miaka sabini, naye alikuwa amepata mimba na alikuwa amzae mwana. Ilikuwa tayari miezi sita akiwa mjamzito. Bila shaka, maskini huyo mtoto mchanga, mtoto Yohana, hakuwa amepata uhai bado, kidogo walikuwa na wasiwasi juu yake.

¹¹² Kwa hiyo tunaona ya kwamba Elisabeti, Zekaria alikuwa mumewe, ambaye alikuwa ku—kuhani, alikuwa hekaluni yapata miezi sita kabla haya hayajatukia. Mwajua, Mungu huyaweka mambo pamoja miongoni mwa watu wanyenyekevu.

¹¹³ Mwangalieni Zekaria, sasa, yule Malaika, Gabrieli, alimjia, alikuwa hekaluni akihudumu, basi alipofanya hivyo, kufukiza uvumba kulikuwa kura yake, akisimama madhabahuni, basi ikatokea aliangalia upande wa kulia, *upande wa kulia* wa madhabahu (Nadhani sikuzote mnashangaa ni kwa nini ninawaleta watu *huku*, ndipo Yeye asimamapo.), kwa hiyo, upande wa kulia wa madhabahu, na hapo alisimama Malaika, na kumwambia ya kwamba baada ya siku za huduma yake kule, ataenda nyumbani na kuwa na mkewe, naye angepata mimba na kuzaa mwana, mtoto.

¹¹⁴ Naye mhubiri huyo akashuku Neno hilo. Mbona, alikuwa mara nyingi, kama alikuwa awe baba wa huyo mtoto, kumwangelia Sara, alikuwa na mifano kadhaa katika Biblia, mwangalieni Hana hekaluni, mifano mingi kama hiyo, na bado alishuku.

¹¹⁵ Ni tofauti jinsi gani na yule mwalimu shupavu wa falsafa, jinsi ilivyokuwa tofauti katika mhudumu huyo wa seminari, kuliko ilivyokuwa katika maskini huyo bikira! Kamwe hakuhoji, alisema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana.” Hivyo tu. Aliamini neno lake, na hilo lilitosha, bali mtu huyu asingeweza kuliadini.

¹¹⁶ Akasema, “Mimi ni Gabrieli asimamaye Mbele za Mungu, neno langu litatimizwa!” Hmm! Alijua alichokuwa anazungumzia. Akasema, “Kwa sababu umenishuku, utakuwa bubu hata siku huyo mtoto atakapozaliwa.” Akaenda nyumbani, mkewe akapata mimba na kujificha, miezi sita.

¹¹⁷ Mariamu akawaza, “Loo, hilo si ni zuri sana? Sasa nitampata mtoto, na hapo Elisabeti, binamu yangu,” Yesu na Yohana walikuwa binamu wa pili, “hapo, nawaambia, itakuwa ni ajabu, kwa sababu yeye atapata mtoto, nami nitapata mtoto. Siwezi kuvumilia zaidi, ninapanda mara moja kwenda kumwambia.” Moja kwa moja akapanda mlimani, upesi alivyoweza kwenda. Ninaweza tu kuuona maskini uso wake mrembo ukimetameta,

alikuwa na umri wa kama miaka kumi na minane tu, nadhani, na nywele zake nyeusi zikipepea nyuma namna *hiyo*. Naye alikuwa njiani, amejifunga joho hili dogo.

¹¹⁸ Nanyi mwajua, Elisabeti alikuwa amejificha. Kwa namna fulani napenda hilo. Nafikiri inaonekana ni fedheha sana kuona wanawake huku nje wamevaa hizi kaptura, na kadhalika, wakati wakiwa na mimba, linaonekana la kusikitisha. Ni tofauti jinsi gani! Inatisha. Ninajua ni... haikupasi... Sipaswi... labda sipaswi kulisema, kama nikiwaudhi, samahani, bali mngemsikiliza daktari wenu, mimi ni ndugu yenu, mnaona.

¹¹⁹ Kwa hiyo huyo hapo mwanamke katika hali hiyo, bali alijificha. Ninaweza kumwazia ameketi kule nyuma, mwajua, kwa namna fulani akipuuzia kidogo, huku, akifuma ninii ndogo, ni kitu gani? Maskini vijibuti, mwajua, kuvitayarisha vyote namna hiyo, na kushona kijiblanketi. Lakini alikuwa anaogopa, kwa sababu alisema, "Sasa, mimi ni mkongwe na..."

¹²⁰ Angalieni, Malaika wa Bwana... Walikuwa wenye haki, Biblia ilisema, yeye na Zekaria, walikuwa wenye haki, wakizishika amri zote za Mungu. Hapo ndipo Malaika wanapoonekana, daima huonekana katika familia yenye haki, mahali fulani ambapo Mungu anaweza kutumia kitu fulani, kitu fulani cha kufanyia kazi.

¹²¹ Halafu basi, alikuwa akitengeneza vijibuti hivi. Nami ninawazia kulikuwako na dirisha dogo, kama ilivyo huko Palestina wakati mwingine, la, haikuwa na taa ndani yake, bali uvuli mdogo tu uking'inia chini, naye akasikia kitu fulani, akasimama na kuangalia akija, naye akasema, "Unajua, ninaamini huyo anaonekana kama binamu yangu Mariamu. Hebu angalia maskini uso wake uking'ara. Mbona, amekua! Nasikia anaenda kuolewa." Kwa hiyo hapana shaka ilikuwa kwamba... "Vema, yeye ni msichana, lakini huyo ni Mariamu." Kwa hiyo haraka anajivika maskini joho lake, mwajua, na kutoka mbio kumlaki.

¹²² Nao wanawake katika siku hizo si kama walivyo siku hizi, mwajua, wao, mimi—mimi... walikimbia na kushikana na kukumbatiana. Mwajua, napenda urafiki, nanyi je? Na—nachukia sana kuona maskini upuuzi huu wa kipumbavu katika aina hii ya urafiki wa mwaka wa 1960. Loo, jamani, hautoshi. Sasa, ninyi mlio watu wa kusini huku chini hamuoni sana, lakini huko juu, loo, jamani!

¹²³ Nilienda kwa mjomba wangu hapa si muda mrefu uliopita huko New York, alikuwa ameishi katika nyumba moja miaka ishirini, naye jirani yake wa karibu kama ile bendera ya Texas *pale*, naye, nami nikasema, "Ni nani anayeishi pale?"

Kasema, "Sijui."

Nikasema, "Umeanguka kutoka kwenye neema." Nikasema, vema nikasema, nikasema, "Basi ameishi hapo muda gani?"

Kasema, “Alikuwa hapo nilipokuja hapa.” Hujui jirani yako amekufa mpaka usome kwenye gazeti. Hiyo ni kweli. Hakuna urafiki.

¹²⁴ Hapa si muda mrefu uliopita, mimi na Ndugu Moore, Ndugu Brown tulishuka kwenda kumwona mvulana mdogo jina lake David, miaka michache iliyopita hapa chini Cali-... , ama, Florida, walitupeleka huko nje. Na—naye Ndugu Hoekstra, naamini ndiye, akaniambia, kasema, “Mwinyi-mke anataka kukuona.”

Nami nikasema, “Ati *nani*?”

Kasema, “Mwinyi-mke.”

Nikasema, “Ni kitu gani hicho?”

Ndipo kasema, “Ni mwanamke anayemiliki mali hii yote.” Kasema, “Yeye ni tajiri.”

“Vema,” nikasema, “siwezi kumwona, kuna wagonjwa wengi kupita kiasi.”

Kasema, “Lakini yeye ni Mwinyi-mke!”

Nikasema, “Hilo halimfanyi tofauti na mtu mwingine yeyote.”

¹²⁵ Kwa hiyo akasema... Vema, walikuwa naye pale nilipotoka nje. Basi nilipotoka nje... Mimi sininii, sasa, Mungu anisamehe kuninii... kama nikininii... mnafikiri ninamdhihaki huyo mwanamke, simdhihaki, lakini alikuwa na vito vya kutosha mikononi mwake kumtuma mmishenari kote ulimwenguni mara kumi, pamoja na Injili. Kama ninii... Akisimama huko nje, naye alikuwa na miwani, hakuwa ameivaa, bali alikuwa ameiveka kwenye kijiti ameishikilia namna *hii*, maskini mama mkubwa mno, mnene, basi akatoka nje.

Nikatoka nje ya hema, nami nikasema, “Vema, sina wakati wa kumwona. Kama nina wakati wowote uliosalia, hebu niwaone hao wagonjwa huko nje,” mnaona.

Kisha kasema, “Lakini yeye alikuruhusu upatumie mahali hapa.”

¹²⁶ Nikasema, “Vema, hilo ni sawa, kama ukimruhusu David apatumie mahali hapa, tunathamini hilo. Lakini yeye ni mzima, hana shida yoyote, hebu niwaone watu hawa hapa chini.”

Vema, walitaka nimwone, kwa hiyo nilipotoka nje, alisema, “Wewe ndiye *Dk. Branham*?”

Nikasema, “La, mama.” Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

¹²⁷ Akasema... Sasa, mnajua hakuna mtu anayeweza kuangalia kupitia miwani iliyo mbali *hivyo* nawe. Naye akaangalia namna *hii*, akasema, “Vema, *Dk. Branham*,” akasema, “*Nimevutiwa*.”

¹²⁸ Nikanyosha mkono, kisha nikautazama mkono huo, nikaunyosha mkono wake kupeana mikono, vema, nikawazia ningekuwa mwungwana, nikaushika mkono wake mkubwa na kuuvuta chini, nikasema, “Ushushe hapa chini nipate kukutambua wakati mwingine nitakapokuona,” namna hiyo. Loo, na—napenda kitu kilicho na hisia!

¹²⁹ Paul Rader, yule mtu aliyeandika wimbo huu ninaoimba hapa, *Amini Tu*, alisema asubuhi moja yeye na mkewe walikuwa na tatizo dogo la familia, wakizozana kidogo, kasema muda si muda mwajua, alikuwa akisoma gazeti, naye mke akasema jambo fulani, “Paul, utanipa pesa kidogo?”

¹³⁰ Kasema, “Sina pesa.” Nao wakaendelea namna hiyo kidogo, kisha kasema baada ya kitambo kidogo, hakutambua kamwe, basi akaumiza hisia zake, kwa namna fulani aliketi pale, na kusema, “Vema, kama hivyo ndivyo hisia zake zinavyoumia kwa urahisi, basi acha aketi hapo.” Mnajua jinsi tunavyofanya, ndugu, wakati mwingine, nadhani.

¹³¹ Na kwa hiyo, basi akasema, yeye...daima angesimama mlangoni na kumbusu alipotoka, kisha angeenda langoni, halafu wakati angegeuka, angempungia mkono kwaheri, naye angempungia mkono kwaheri. Kasema alisimama, akachukua kofia yake, na kusema, “Acha tu abibidue midomo.” Kasema alienda mlangoni, na kusema, akatoa midomo yake, akambusu, akafika hata mwisho wa lango, akageuka na kuangalia nyuma, kasema alikuwa amesimama mlangoni, kasema alimpungia mkono, naye akampungia mkono.

¹³² Kasema alianza kushuka barabarani kisha kasema *Kitu fulani* kikaanza kumshughulikia, “Umekosea, Paul.” Maskini mzee Paul yuko Utukufuni usiku wa leo. Lakini kasema, “Umekosea, Paul. Vipi kama jambo fulani lingempata leo?” Kasema alianza kuwazia hilo. “Loo, jamani, vipi kama jambo fulani lingetukia? Hungemwona tena duniani.” Loo, jamani!

¹³³ Kasema alizidi kusikia vibaya, vibaya, kisha akasema, “Bwana, nisamehe, nitarudi nikalirekebishe.” Kasema akarudi mbio, akafungua lango, akafungua mlango kwa nguvu, akaangalia kote, angeweza kusikia kitu fulani kikifanya, “*kuvuta kamasini ndani, kuvuta kamasini ndani.*” Naye akasema alikuwa amesimama nyuma ya mlango, akilia.

¹³⁴ Kasema alinyosha mkono, hakusema neno, akafanya, “*busu,*” akambusu tena, akarudi mbio hadi mwisho wa lango, kisha akageuka, akapunga mkono, akasema naye akapunga mkono, kama tu alivyofanya mara ya kwanza, lakini akasema, mara ya pili ilikuwa na hisia ndani yake. Kwa hiyo, nafikiri hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, tunataka ninii...Ninataka hisia ndani yake, kitu ambacho ni halisi kwangu.

Nilikuwa, si muda mrefu uliopita, mimi na mke wangu tulikuwa katikati ya mji, kulikuwa na mama mmoja aliyesema, “U hali gani, Dada Branham?”

Ndipo nikageuka nikamtazama, nikasema, “Hei, hei! Huyu mama alikuzungumzia, Mpenzi.”

Kasema, “Nilizungumza naye.”

Nikasema, “Vema, ninajua yeye hakukusikia, mimi sikukusikia, nimeketi papa hapa karibu nawe.”

“Loo,” akasema, “Nilimwitikia kwa tabasamu.”

“Loo,” nikasema . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

135 Akasema, “Unajua, Mariamu, mimi ni mjamzito.”

“Loo, naam, naam,” akasema Mariamu, macho yake madogo yakimetameta, mwajua, huku yamejaa nusu machozi ya furaha, “naam, naam, ninajua yote kulihusu.”

“Ati unajua yote kulihusu?”

“Naam, naam, ninajua yote kulihusu.”

136 “Vema, lakini Mariamu, ninasumbuka, ni miezi sita nikiwa na mimba sasa, wala huyu mtoto mchanga kamwe hajasogea.” Sasa mnajua, hayo—hayo si ya kawaida kabisa. Yapata miezi mitatu karibu ni sawa, lakini hii ni miezi sita, wala mtoto John hakuwa amesogea bado. Kwa hiyo, akasema, “Nina wasiwasi kidogo juu yake na kadhalika.”

Akasema, “Naam, na—naelewa hilo.” Kisha kasema, “Unajua, nitapata Mtoto, pia.”

“Loo, kumbe, wewe na Yusufu tayari mmefunga ndoa?”

“La, hatujafunga ndoa.”

“Ati nini, Mariamu? Hujaolewa, na ati utapata Mtoto?”

“Naam, hiyo ni kweli.”

“Loo, Mpenzi, unamaanisha nini?”

137 “Vema, vile vile nilivyojua ya kwamba utampata mtoto, Malaika Gabrieli alikutana nami, naye akaniambia kuhusu kisa chako, naye akasema Roho Mtakatifu angekuja juu yangu, na tayari amenijilia. Naye Mtoto mchanga nitakayempata atakuwa ni Mwana wa Mungu.” Kisha kasema, “Hata aliniambia . . . Yeye aliniambia nitamwitaje.” Kasema, “Nitamwita Jina Lake Yesu.”

138 Nami ninaweza kuona uso wa Elisabeti ukichangamka, kasema, “Imetokeaje mama wa Bwana wangu kunijilia? Maana mara sauti ya kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto changu kichanga kikaruka kwa furaha tumboni.”

139 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani, enyi marafiki: Ikiwa mara ya kwanza ambapo Jina la Yesu Kristo lilipata kutajwa kwa midomo ya mwanadamu kulikifufua kitoto kichanga kilichokufa tumboni mwa mama, linapaswa kufanya nini

kwa kusanyiko la Mungu lililozaliwa mara ya pili, linalodai kujazwa na Roho Mtakatifu? Haleluya! Amina! Linapaswa kuponya kansa, kuyafungua macho yaliyopofuka, kuwaweka huru waliojeruhiwa, kuwajaza na Roho Mtakatifu, kufanya mambo ya kila namna, Jina hilo la thamani la Bwana Yesu, kumfanya mwenye dhambi azililie dhambi zake. Loo, jamani!

¹⁴⁰ Umati wote unaonekana kwangu kana kwamba unaogelea kuzunguka, na kuzunguka. Loo, kile Mungu angeweza kufanya sasa hivi! Mjumbe wa Roho Mtakatifu wa Mungu yuko humu jengoni leo, yule Mjumbe, Roho Mtakatifu, akileta amani, akimwakisi Yesu Kristo. Ile Nguzo kuu ya Moto inaning'inia juu yetu.

Unasema, “Siioni.”

¹⁴¹ Unaweza kuihisi, kwa hiyo hisi yako moja—moja ya mwili ni sawa tu na ile nyingine. Kwa hiyo, macho yako yangeweza kukudanganya kuliko hisia zako. Kwa hiyo basi kama hafanyi kazi ile ile, basi si Roho Mtakatifu yeye yule; lakini kama akifanya kazi ile ile, basi ni Roho Mtakatifu, Yule yule. Amina. Unaamini hilo?

¹⁴² Wangapi...? Je, kuna wenye dhambi? Ni wangapi hapa ndani wangetaka kusema, “Ningependa kufurahia baraka hizi, kuketi katika Utukufu huu wa Shekina pamoja nanyi watu na kufurahia baraka za Mungu”? Waweza kuinua mkono wako? Sema, “Unikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba.” Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, Ndugu, wewe, huko, na wewe na wewe. Hiyo ni kweli. Mwingine inua mkono wako, useme, “Ndugu Branham, uniombee.” Mungu akubariki, ewe kijana. Hilo ni zuri sana.

¹⁴³ Asubuhi ya leo nilipokuwa nikienda kwenye kiamshakinywa maskini mvulana mdogo alikuja akanikumbatia shingoni. Baba yake ni mmoja wa wachungaji hapa wa Assemblies of God, ninaamini yuko jukwaani, alikuwako asubuhi ya leo. Naye huyo mvulana mdogo akaitwa mikutanoni mahali fulani, naye alikuwa na macho yenye makengeza, ndipo maskini macho yake yakanyoka kama yangu, hiyo imekuwa miaka mingi iliyopita.

¹⁴⁴ Ndipo maskini ndugu mwingine akaja na kunipa mkono, kasema msichana wake mdogo alikuwa na tezi kubwa mno kooni mwake nilipokuwa huko chini kwenye kanisa la Jack Moore, na kusema Roho Mtakatifu alizunguka kote, na kumwita huko nje kwenye kusanyiko, na kumwambia ya kwamba hiyo tezi ndio kwanza iondoke na kutoweka na kumtoka; huyo hapo. Loo, jamani!

¹⁴⁵ Ni kitu gani? Nguzo hiyo ya Moto ni nini? Ni Malaika wa Bwana. Malaika wa Bwana ni nini? Yeye yule aliyekuwa katika kichaka kilichowaka moto, Yeye yule aliyekuwa katika Yesu

Kristo, Yeye yule aliye ndani yenu usiku wa leo. Amina. Yeye yule hapa, Bwana Yesu yeye yule aliye mkuu.

¹⁴⁶ Kunaweza kuwa na mwingine, kabla hatujaomba, ungetaka kuinua mikono yako, na kusema, “Nikumbuke, Ndugu Branham, nikumbuke”? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, na huyo mvulana mdogo huko nyuma kabisa, na mbali huko nje, nyuma kabisa. Naam. Popote ulipo, Mungu anajua.

¹⁴⁷ Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Na sasa, Dada, waweza kunipigia huu: *Tabibu Mkuu Sasa Yu Karibu?* Sauti yake tu, ukipenda, tafadhali, Dada.

¹⁴⁸ Ninakumbuka karibu na Fort Wayne, ama, ilikuwa huko Fort Wayne, Indiana, nimekuwa mimbarani, sasa, miaka thelathini na mmoja, hii imekuwa kama miaka ishirini na minane iliyopita, nilikuwa nikimwomba mvulana mdogo, na muziki huo ulikuwa ukiendelea. Mvulana huyo mdogo akaponywa, akaruka kutoka mikononi mwangu, aliyepooza, akakimbia chini, akaruka mikononi mwa mama yake.

¹⁴⁹ Basi alipofanya hivyo, maskini msichana mdogo wa Dunkard alikuwa akipiga pi—piano, naye akasimama, nywele hizo zikaangukia pajani mwake, namna *hiyo*, akaanza kuimba katika Roho, nacho hicho kina-... , ama, piano aliyokuwa akipiga, huku hivyo vibao vya pembe za ndovu vikiendelea kujipiga, “Tabibu mkuu sasa yu karibu, Yesu mwenye huruma,” mamia ya watu wamesimama wakiiangalia.

¹⁵⁰ Si zaidi hata kidogo ilikuwa Jumapili iliyotangulia hii iliyopita katika Maskani yangu, ambapo watu mia tatu hadi mia nne wakisimama pale, ndipo Nguzo hii ya Moto ikaonekana mara ya pili huko Jeffersonville. Mara ya kwanza walipoipiga picha huko chini mtoni. Naye hapo akasimama kwa dakika kumi na tano, akimruhusu kila mtu amwone na kumwangelia. Ndugu, tuko kwenye mwisho wa safari.

¹⁵¹ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja sasa, Bwana, Kwako kama kwenye Jiwe lililo hai. Tunakuja, Bwana, kwa sababu tunaamini ya kwamba Wewe upo, na Mtoa thawabu kwa wale wanaokutafuta Wewe kwa bidii. Tunaomba kwa ajili ya baraka Zako, tunaomba ya kwamba utalisaidia kusanyiko hili usiku wa leo. Na wale walioinua mikono yao, jalia wawe washiriki wa huyu Roho Mtakatifu mkuu, Mjumbe wa siku ya mwisho.

¹⁵² “Nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.” Uliahidi jambo hilo. Katika siku za mwisho Wewe ulisema kutakuwa na mvua ya masika na mvua ya vuli pamoja, yaani, upande mmoja wa dunia na upande mwingine wa dunia, pande zote mbili, mvua itakuja, kwenye maeneo ya kigeni, kwenye maeneo haya ingenyesha mvua. Kwa hiyo, tunaamini ya kwamba saa hiyo imewadia. Tunamwona Roho Mtakatifu akidhihirisha mambo yale yale kama Yeye alivyofanya alipokuwa hapa hapo kabla.

¹⁵³ Wabariki watu hawa wapendwa, Baba, ninaomba, uwe karibu nao, uwape Uzima wa Milele. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Bwana Yesu.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na tuombe tu kidogo.

... Tabibu sasa yu karibu,
Yesu mwenye huruma;
Yeye hunena akauchangamsha moyo
uliohuzunika,

¹⁵⁴ Loo, tupumulie, Roho Mtakatifu. Ingia kanisani Mwako, Bwana Yesu, ile Nyota kuu ya Asubuhi, ile Nguzo ya Moto, choma njia Yako katika kila kutokuamini katika mioyo ya watu, usiku wa leo. Jalia wawe kama Mariamu, hata waweze kuuona Uwepo Wako na kujua ni Wewe, basi ahadi Zako zingali ni nzuri, kila ahadi. Uliahidi kufanya jambo hili. Ahadi Yako ilikuwa kwamba ulikuwa tayari umewaponya, kwa—kwa kuwa ulijeruhiwa kwa makosa yao, na kwa hayo mapigo uliponywa. Lijalie, Baba, kwa kusanyiko hili linalongojea. Tunakungojea Wewe sasa. Tenda kazi, katika Jina la Kristo, ninaomba.

¹⁵⁵ Naangalia tu kwa dakika chache, nione kitakachotukia. Loo, ni tamu jinsi gani! Na tuinue vichwa vyetu kwa urahisi sana sasa. Nilikuwa nikiwangojea mtulie. Ni watu wangapi humu ndani ambao ni wagonjwa, wala hawana kadi ya maombi, inueni mikono yenu, mnaotaka Mungu awaponye. Thibitisho ni watatu, naamini. Hiyo ni kweli, katika Biblia? Kama nimesema kweli, nikahubiri kweli, basi Mungu anawajibika kuiunga mkono kweli hiyo, kama hiyo ni kweli Yake.

¹⁵⁶ Sasa, tuna lundo la kadi za maombi hapa ndani, hatuwaiti, ninawatakeni tu mjue ya kwamba haihitaji kadi za maombi. Waulizeni wahudumu kama inahitaji, waulizeni ndugu wanaoambatana nami kila mahali.

¹⁵⁷ Tutakuwa tukiendesha gari barabarani, nitasema, “Ngojeni! Kwenye kona nyingine litatokea jambo *fulani*, mtu atakuwa amesimama pale, ana kitu *fulani*, anataka niende mahali *fulani* kwenye kitu *fulani*. Tunaenda *huku*, *hili* litatukia.” Hakika, kamwe halishindwi. Kamwe haliwezi kushindwa, ni Mungu. Sasa, inafanya nini? Inathibitisha ya kwamba Yeye ni yeye yule. Sasa si mimi, ni Yeye.

¹⁵⁸ Sioni mtu mbele yangu ninayemjua, isipokuwa iwe ni wasichana hawa wawili wadogo, aisee, ninaamini hawa ni wasichana wawili wa Ndugu Evans. Sivyoy? Papa hapa. Hao ndio tu ninaowafahamu. Nilikuwa nikiangalia tu kuona kama ningeweza kumwona mtu yeyote ambaye kweli nilimjua. Lakini mimi, wale tu ninaoona ninawajua, nilimwona Ndugu Evans mahali fulani muda mfupi uliopita, bali nimempoteza.

¹⁵⁹ Loo, naam, huyu hapa Ndugu Dauch, aliyeketi papa hapa, kutoka Ohio, Ndugu Bill Dauch, rafiki yangu, aliyeketi papa

hapa, na Dada Dauch. Yule pale Dada Evans, sasa nimemwona, pale pale nyuma, vema, moja kwa moja mle ndani, Ndugu Evans, ama, Dada Evans. Yuko wapi Ndugu Welch? Ameketi kule nyuma. Vema. Ili kwamba wajue ninyi nyote ni akina nani, inua mkono wako.

Mtu yeyote hapa ndani anayenijua, na unayejua ya kwamba ninakujua, inua mikono yako, unajua ya kwamba mimi—kwamba ninakujua. Vema. Vema, mnaona.

¹⁶⁰ Sasa wewe unayejua ya kwamba sikujui, nawe ni mgonjwa, inua mkono wako, inua mkono wako. Angalieni tu mwone mahali walipo, mnaona. Karibu kila mahali. Vema.

¹⁶¹ Kama ninii... Ikiwa Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Biblia ilisema ya kwamba hapo mwanzo kulikuwako Neno naye Neno alikuwa Mungu. Hiyo ni kweli? Naye Neno alifanyika mwili. Hapo ndipo Neno la Mungu alilonena, lilipofanyika mwili.

¹⁶² Je, unajua mavumbi yenyewe unayokalia ni dhihirisho la Neno la Mungu? Hayo ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Kama sivyo, yalitoka wapi? Aliufanya ulimwengu kwa vitu visivyoonekana. Mnaona? Aliumba dunia pamoja, akanena tu Neno, na kusema, “Na iwe,” na ikawa, Yeye ni Muumba. Vema. Kwa hiyo kiti unachokalia ni Neno la Mungu, udongo unaokaliwa na sakafu ni Neno la Mungu, vitu hivi vyote vimetokana na mavumbi ya nchi, Neno la Mungu, na wewe, mwenyewe, ni Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Basi kwa nini maskini moyo huo humo ndani usiweze kuanza kuondoa shaka yote kutoka kwenye kitu hiki hapa. Na iwe hivyo.

¹⁶³ Sasa, nalo Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wowote ukatao kuwili, huchoma hata kufikia mafuta ya mfupa, na kugawanya na mafuta ya mfupa, nalo Neno la Mungu, ambalo ni Yesu, ni Mpambanuzi wa mawazo yaliyomo ndani ya moyo na nia. Hiyo ni kweli?

¹⁶⁴ Sasa, wakati Neno lilipokuwa hapa, na kufanyika mwili, na kukaa kwetu katika umbo la Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, maskini mwanamke mmoja, kwa imani, aligusa vazi Lake siku moja, hakukuhisi kimwili, bali aligeuka, akaangalia, akasema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?”

Hata Petro akamkemea, kasema, “Bwana, kila mtu anakugusa.”

¹⁶⁵ Akasema, “Naam, lakini ni—ni—niliona, Mimi, nguvu zilinitoka, nikawa dhaifu, nguvu Zangu ziliniacha.” Naye akasema, akaangalia kote kwenye kusanyiko, ndipo akamwona maskini mwanamke huyo, akamwambia, kutokwa kwake na damu alikokuwa nako, imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli? Aliponywa. Kamwe hakusema, “Nilifanya hivyo.” Mwanamke huyo alifanya hilo yeye mwenyewe. Mnaona? Kasema, “Imani yako imeokoa...”

¹⁶⁶ Sasa, Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele; nacho Kitabu cha Waebrania kinasema ya kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, ukimgusa Kuhani Mkuu yuyo huyo, Kuhani Mkuu yuyo huyo atatenda vivyo hivyo. Jinsi alivyotenda mara ya kwanza inambidi kutenda mara ya pili, kama hakufanya hivyo, alikosea alipofanya hivyo mara ya kwanza.

¹⁶⁷ Kama Yeye alijitambulisha Mwenyewe kama Masihi kwa Wayahudi na Wasamaria kwa kuyatambua mawazo niani mwao, na kuwaambia wao walikuwa ni akina nani, ama kile walichokuwa, na kadhalika namna hiyo, na jambo fulani walilokuwa wamefanya (Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli, hiyo—hiyo ni kweli ya Biblia, hivyo ndivyo alivyojifanya Mwenyewe...?), vema, kama hivyo ndivyo alivyolitambulisha kwa Wayahudi na Wasamaria, hana budi kulitambulisha kwa Mataifa, la sivyo alilitambulisha kwao vibaya. Mnaona ninalomaanisha?

¹⁶⁸ Sasa, wote wanaoamini hilo, inua mkono wako, useme, “Ninaamini ya kwamba Yeye aliliahidi, nami ninaamini.” Asanteni. Hilo lilitosha. Mnaona, kumbukeni vile Malaika alivyosema, “Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini?” Mnaona? Sio kuniamini mimi kuwa ni Yeye, bali kuamini ya kwamba Yeye alinituma kwenu. Sasa, wewe omba na umguse Kuhani Mkuu. Na kama atanigeuza kutoka kwenye jukwaa hili, na kusema nawe, hebu... wewe uwe mwamuzi kama ni kweli ama si kweli. Wewe kuwa mwamuzi kama ni kweli ama si kweli.

¹⁶⁹ Sema tu, sasa, angalia mbali nami kama mwanadamu, na useme, “Bwana Yesu, nina haja.” Wala usijaribu kujisukumiza, hufiki popote basi, tulia tu, useme, “Ninaamini, Bwana, sina shaka niani mwangu. Huyu mtu hanijui, nami niko mbali sana naye, niko hapa nje kwenye kusanyiko,” mbali kabisa huku nyuma, ama kusimama kuzunguka huu ulingo, ama mahali fulani namna hiyo. “Sasa, najua ninakuamini. Kama utaniruhusu tu nikuguse, jalia anigeukie, nitajua ya kwamba huyo si Ndugu Branham, kwa sababu yeye hanijui, wala hajui ni nini, mimi ni nani, ama nimefanya nini, ama, kile nimefanya, ama kile nitakachofanya, bali Wewe unajua jambo hilo, kwa hiyo kama utamruhusu tu ageuke, ninajua ni Wewe. Nitaamini Ujumbe wake basi, kwa sababu Wewe unamwongoza,” mnaona, “ni Wewe ukinena kupitia kwake.” Mnaona?

¹⁷⁰ Mngeamini hilo? Ni wangapi wangeamini kama wangeliona likitendeka kwa macho yao wenyewe? Hebu tuone. Si huko nyuma kwenye chumba fulani chenye giza, papa hapa mbele ya umma, kama vile Bwana wetu alivyosimama. Msiwe na... Si kitu cha kisiri, ni papa hapa nje, ni kwa ajili ya waaminio tu. Sasa, ninyi ombeni tu.

¹⁷¹ Huenda nilikosea, nilifikiri ilikuwa mahali fulani papa hapa, lakini bila shaka haikuwako. Ninaiangalia, ni Nuru tu. Hivi upande huu waliinua mikono yao kwamba walikuwa wagonjwa, pia, wala hawakunijua mimi? Sasa, Yeye yuko papa hapa. Ninyi mnaoziangalia hizo picha, na kadhalika, wazienu tu, hilo jicho la kimitambo la picha liliiona kabla watu wengi hawajaiona, kaipiga picha. Kama nikifa usiku wa leo, endapo hii ndiyo siku yangu ya mwisho duniani, ushuhuda wangu ni wa kweli. Jicho la kimitambo la kamera limeithibitisha mara saba ama nane katika mataifa mbalimbali. Ni kweli, Kanisa linajua jambo hilo kote ulimwenguni.

¹⁷² Nimesema kweli, mimi, kwa sababu ninanena habari Zake. Hiyo ndiyo sababu siogopi kwa kuwa Yeye atanena tena kwamba nilisema kweli, kwa sababu sijishuhudii mwenyewe, ninamshuhudia Yeye. Sasa iweni na kicho kabisa, na mwamini.

Unasema, “Unangojea nini, Ndugu Branham?”

Ninamngojea Yeye. Asiponiambia, siwezi kufanya hivyo, hivyo tu. Inahitaji imani yako kufanya jambo fulani. Ama labda Yeye hafurahishwi na sisi kufanya hivyo.

¹⁷³ Ni wangapi walio na kadi za maombi basi? Kama wewe...? Kuna mtu aliye na kadi za maombi? Kadi moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, takriban kadi nane za maombi zimesalia, tisa. Tutawaita asipofanya hivyo. Ninapenda kuona hilo likifanywa bila kadi za maombi, mpate kuona kadi ya maombi haina uhusiano wowote nalo.

¹⁷⁴ Mungu, tusaide usiku wa leo. Sasa ninaomba ya kwamba utatujalia. Nimekuja hapa kwa nia njema, nimekuja hapa nikiamini, nikiamini ya kwamba Wewe ungefanya hivyo. Ninaomba ya kwamba utanisaidia sasa. Nipe Roho Wako, Bwana. Tujalie, ili iweze kuwa kwa utukufu Wako. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁷⁵ Naam, Hii hapa. Asante, Bwana. Unaamini Mungu atakuponya hiyo ngiri, mama, akupe afya? Vema. Likubali. Inua mkono wako. Vema. Je, una kadi ya maombi? Huna. Huihitaji.

Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu.

¹⁷⁶ Hivi hatufahamiani, Dada mpendwa? Sikujui. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili kusanyiko liweze kuona. Hiyo ilikuwa ndiyo shida yako? Ulikuwa umeketi pale ukiomba, sivyo? Sasa nimepata mawasiliano yako. Ulikuwa ukimwomba Yesu, “Jalia iwe ni mimi.” Hiyo ni kweli? Punga mkono wako namna *hiyo*. Inua mkono wako, naam, vema, punga mkono wako, wapate kuona.

Sasa, nilijuaje kile alichokuwa akiombea, na maneno aliyokuwa akisema? Mnaona? Hivi hamwoni? Ni Kristo.

¹⁷⁷ Hapa, maskini mama mmoja sasa hivi alijisogeza, aliyeketi pale sasa. Unataka kuondokana na ugonjwa huo wa moyo, Dada? Haikubidi kuja hapa juu, angalia tu *huku*. Unataka kuondokana na ugonjwa wako wa moyo? Vema. Inua mkono wako, useme, “Ninalikubali.” Vema, nenda nyumbani, ugonjwa wako wa moyo umekwisha, Yesu Kristo anakuponya.

¹⁷⁸ Maskini mama aliyeketi moja kwa moja nyuma yake, una shida ya kike. Simama kama hiyo ni kweli. Vema. Je, una kadi ya maombi? U—una moja? Sikukusudia kukuita. Vema. Nenda nyumbani. Wewe ni... ulikuwa... ulikuwa unasumbuliwa na macho yako, yanaharibika, pia. Hiyo ni kweli? Punga mkono wako. Si kwa sababu umevaa miwani, bali yanazidi kuharibika. Vema. Hayataharibika tena sasa. Nenda zako nyumbani, Yesu Kristo anakuponya.

¹⁷⁹ Aisee, nipe fadhili, utafanya hivyo? Wapate kujua, kwa kuwa ulikuwa na kadi, huyo mama aliyeketi hapo karibu nawe, yeye, upande huu hapa, akiugua hapo kwa tezi, unaamini ya kwamba Yesu Kristo atakuponya? Ni tezi ya ndani, lakini hiyo ni sawa, amini, naye itakuondokea. Vema.

¹⁸⁰ Sasa, kama unaamini mimi ni nabii wa Mungu, weka mkono wako juu ya mwanamke aliye karibu nawe, akilia hapo, Malaika wa Bwana yuko juu yake. Ana shida na kichwa chake. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako mama, yule niliyemwita basi. Vema. Simama kama hiyo ni kweli, yule aliye na lesa mkononi mwake. Vema. Yesu Kristo anakuponya, nenda nyumbani, uponywe.

¹⁸¹ Unamwamini Yeye? Sasa, je, huyo Malaika ni wa Kimaandiko? Hapa, huku nyuma kabisa, Huyo hapo nyuma kabisa, kuelekea, huko nyuma kabisa. Huyo hapo mtu na mkewe, mke ana kisukari, mwanamume ana yabisi kavu. Loo, laiti ningeweza tu kuwafanya waelewe! Mungu, nisaide. Bw. na Bibi Wilkerson, simameni kwa miguu yenu, Yesu Kristo anawaponya. Nendeni nyumbani mkapate afya, Kristo anawaponya.

¹⁸² Je, una kadi ya maombi? Huna? Huna moja, huhitaji yoyote. Mnaposimama kwa miguu yenu, sikilizeni hili, enyi marafiki, siwajui ninyi nyote, sivyo? Kama sikujui, itikise mikono yako huku na huku. Mnaona? Sikujui. Ulikuwa umeketi pale ukiomba. Hiyo ni kweli? Jambo fulani limekupata. Hiyo ni kweli? Vema. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako? Je, hilo ndilo jina lako? Yote aliyosema ni kweli? Punga mkono wako nyuma namna *hii*, kama ni kweli. Punga mkono wako. Vema. Haya basi. Nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya.

¹⁸³ Waligusa nini? Mnaamini Malaika aliye mbele yetu, ni Malaika wa Mungu? Sio mimi. Siwajui hao watu, ninashuhudia, wanashuhudia, hatufahamiani, kwa hiyo haina budi kuwa ni Malaika wa Bwana. Naye anafanya mambo yale yale ya

Kimaandiko ambayo Yesu alisema angefanya kabla tu ya kuteketezwa kama Sodoma. Amina!

Hebu tuone. Kama mtaamini!

¹⁸⁴ Hapa, Hii hapa tena, papa hapa pembeni. Ngoja, ni yule mama, la. Sasa, hebu kidogo tu. La, si yule mama aliyesimama pale, ni huyu mama aliyeketi hapa chini. Hiyo ni kweli, maskini mama aliyeketi hapa, nimemwona mtoto, lakini ni mama aliyeketi chini, naye anaugua bawasiri. Naye, huyo ni msichana wake mdogo aliyeketi hapo, anaugua pumu. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, Yesu Kristo anakuponya. Simameni, nyote wawili. Kama hatufahamiani, inueni mikono yenu, na kupunga mikono yenu. Vema. Nenda nyumbani, mpenzi, yote yamekwisha, msichana mdogo. Ninyi nyote mponywe.

¹⁸⁵ Mnaamini? Angalieni *hapa*, angalieni *hapa*, angalieni *hapa*, *hapa*, *hapa*! Hivi hamwezi kuiona hiyo, Ndugu Jack? Angalieni *hapa*! [Ndugu Jack anasema, “Loo, naam!”—Mh.] Papa *hapa*, imesimama moja kwa moja juu ya mtu huyu hapa. Huyu mtu anaugua ngiri. Hiyo ni kweli. Yeye hatoki humu mjini, anatoka mji uitwao Orange. Hiyo ni kweli. Jina lake ni Bw. Sack. Hiyo ni kweli, bwana? Endapo mimi ni mgeni kwako, pungu mikono yako nyuma na mbele, namna *hii*. Ulikuwa umeketi pale, ukisema, “Na iwe ni mimi, Bwana.” Hiyo ni kweli? Punga mkono wako.

¹⁸⁶ Ee Mungu! Unawezaje kukosa kuliona? Ninamwamuru kila mgonjwa humu ndani kusimama kwa miguu yako na kupokea uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Simameni, msio gope. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote. Katika Jina la Yesu!...?... 

61-0121 Imani Ya Mariamu
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org